



**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2**  
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2**  
**SUAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2**

Wednesday 16 May 2007 (morning)  
Mercredi 16 mai 2007 (matin)  
Miércoles 16 de mayo de 2007 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2<sup>e</sup> partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à amener des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.
- No se permite traer a la sala de examen copias de las obras estudiadas.

Jibu swali **moja** tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo ambao umejitayarisha nao. Majibu ambayo **hayana** mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 **hayatapewa** alama nyingi.

### **Tamthilia**

#### **1. Ama**

- (a) Kwa kuzingatia angalau kazi mbili ulizozisoma jadili jinsi waandishi uliowateua wanavyozingatia migogoro inayojitokeza katika kuendeleza utu na uonyeshe pingamizi zinazojitokeza katika kuukuza.

*Au*

- (b) Waandishi wa kazi za fasihi wanatumia mbinu mbali mbali ili kufanikisha upitishaji wa ujumbe wao. Jadili kwa undani mikakati anayoitumia mwandishi na uonyeshe inavyochangia katika kufanikisha kazi za tamthilia.

### **Riwaya**

#### **2. Ama**

- (a) Ni kwa vipengele na azma ipi waandishi wa kazi ulizozisoma wanavyozungumzia kuhusu swala nyeti la ukinzano uliopo baina ya matabaka mbalimbali katika jamii.

*Au*

- (b) Kwa kuzingatia kazi ulizozisoma linganisha jinsi waandishi wa kazi za riwaya wanavyoendeleza hisia za vitisho katika kuleta mahangaiko kwa wasomi na wahusika katika kazi hizi.

### **Ushairi**

#### **3. Ama**

- (a) Kwa kuzingatia mashairi mawili au matatu kutoka kwenye kazi ulizozisoma linganisha jinsi ushairi huu unavyochochea hisia, kuamsha ari na kutoa msisimko.

*Au*

- (b) Linganisha matumizi na athari ya miundo mbalimbali ya ushairi kama inavyotumiwa na washairi mbalimbali. Zingatia kazi ulizozisoma katika mjadala wako.

## Riwaya ya mapenzi

### 4. *Ama*

- (a) Jadili kwa mapana na marefu kuhusu athari za lugha ya mapenzi katika kuleta mgawanyiko katika jamii ya kisasa na tamaduni za jadi. Zingatia kazi ulizojitayarishia.

*Au*

- (b) Linganisha njia ambazo wasanii mbalimbali wanavyosawiri utata uliopo katika ndoa katika kazi mbili ulizosoma. Onyesha ni usawirishaji upi wa ndoa kama msomaji unaokuridhisha na kwa nini?

## Maswali ya kijumla

### 5. *Ama*

- (a) Ni kwa njia na madhumuni yapi waandishi katika kazi ulizozisoma wanavyoonyesha umuhimu wa ustawi wa watoto katika kazi zao.

*Au*

- (b) Jadili kwa kuzingatia kazi ulizozisoma umuhimu wa ndoto na imani katika kazi za wasanii.

*Au*

- (c) Jadili ni kwa vipengele vipi waandishi katika kazi ulizozisoma wanavyosisitiza au kutoa changamoto kuhusu swala la utambuzi.

*Au*

- (d) Wasanii wengi huandika kuhusu yale waliyoyasikia, kuyaona na yaliyo kwenye akilini na kuzingatia hadhira yao katika utunzi wao. Jadili ukweli wa kauli hii ukizingatia kazi ulizozisoma.